TANGAZO LA SERIKALI NA 448S la tarehe 30/6/2023

SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA,
(SURA YA 51)

**KANUNI**

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 36(1) na (2))*

KANUNI ZA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
USAJILI WA WATOA HUDUMA ZA UTAFITI WA KILIMO NA MIRADI YA UTAFITI

*(a) Usajili wa Watoa Huduma za Utafiti wa Kilimo*

4. Usajili wa watoa huduma za utafiti wa kilimo.
5. Uamuzi wa maombi.
6. Ada ya kuhuisha cheti cha uendeshaji.
7. Rejesta ya watoa huduma za utafiti wa kilimo.

*(b) Usajili wa Miradi ya Utafiti wa Kilimo*

8. Utaratibu wa usajili na uidhinishaji miradi ya utafiti wa kilimo na watafiti katika sekta binafsi.
9. Uchambuzi wa andiko.
10. Kuongeza muda.
11. Rejesta ya miradi ya utafiti wa kilimo.
12. Mradi wa utafiti wa taasisi ya umma.

*TANGAZO LA SERIKALI NA 448S (Linaendelea)*

13. Kuwasilisha ripoti za utafiti.

SEHEMU YA TATU
TAARIFA NA TAKWIMU ZA UTAFITI WA KILIMO

14. Utunzaji na usalama wa takwimu.
15. Kuanzisha mfumo wa taarifa jumuishi.

SEHEMU YA NNE
MFUKO WA MAENDELEO YA UTAFITI WA KILIMO

16. Matumizi ya Mfuko wa Maendeleo ya Utafiti wa Kilimo.
17. Kuanzishwa kwa Kamati.
18. Majukumu ya Kamati.
19. Akaunti na Ukaguzi wa Mfuko.

SEHEMU YA TANO
UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

20. Kuwasilisha malalamiko.
21. Kukataa malalamiko.
22. Ukomo wa muda.
23. Mahudhurio ya pande husika.
24. Uwasilishaji wa hati ya mashtaka.
25. Usikilizaji wa malalamiko.
26. Matokeo na mapendekezo.
27. Uamuzi wa Taasisi.
28. Kumbukumbu za mwenendo wa mashauri.
29. Rufaa kwa Waziri.
30. Uwasilishaji wa rufaa.
31. Uthibitisho wa uwasilishaji wa nyaraka.
32. Mamlaka ya Waziri.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MBALIMBALI

33. Uzalishaji na matumizi ya mbegu.
34. Jukwaa la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo.
35. Makosa na adhabu.

______________

**MAJEDWALI**

______________

TANGAZO LA SERIKALI NA 448S la tarehe 30/6/2023

SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA,
(SURA YA 51)

## KANUNI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 36(1) na (2))*

KANUNI ZA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA ZA MWAKA 2023

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania za Mwaka 2023.

Matumizi

**2.** Kanuni hizi zitatumika Tanzania Bara;

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 51

“Sheria” maana yake ni Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania;

"habari" maana yake ni takwimu zilizochambuliwa na kutathminiwa ambazo zinaweza kuwasilishwa katika muundo tofauti;

"ugunduzi wa kilimo na ugunzi wa kisayansi unaohusiana" maana yake ni mchakato au bidhaa ya uchunguzi wa kisayansi wenye mafanikio;

"teknolojia" maana yake ni matumizi ya mbinu bora katika kilimo kwa lengo la kuongeza tija, ikijumuisha matumizi ya aina mpya za mbegu zilizoboreshwa na kanuni bora za kilimo;

"mradi wa utafiti wa kilimo" maana yake ni huduma za kisayansi ambazo zimepangwa kwa uangalifu na muda maalum kwa lengo la kutatua vikwazo katika kilimo kwenye mnyororo wa thamani wa bidhaa unahusisha uzalishaji, kuongeza thamani, masoko, ulaji na matumizi;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya

Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria;

Sura ya 346

"taasisi ya umma" maana yake ni taasisi yoyote ya utafiti, iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu au sheria nyingine yoyote;

"cheti cha usajili" maana yake ni hati rasmi inayothibitisha kuwa mtu au kampuni imewasilisha taarifa zote muhimu kwa kumbukumbu rasmi za Taasisi;

"cheti cha uendeshaji" maana yake ni hati rasmi inayoonyesha kuwa mtu ana sifa za kutosha kufanya kazi kama mtoa huduma wa utafiti wa kilimo;

"huduma" maana yake ni utoaji wa huduma kama vile ushauri elekezi, mafunzo, huduma za maabara, kukodisha mashine, ukodishaji wa ardhi na huduma zingine zinazohusiana;

"bidhaa za utafiti" maana yake ni teknolojia na ubunifu unaotokana na utafiti wa kilimo kama vile kanuni bora za kilimo, mbegu, bidhaa zilizoongezwa thamani, zana za msaada wa maamuzi, aina ya mapishi, itifaki za kisayansi na bidhaa zingine zinazohusiana;

Sura ya 308

"mbegu" maana yake ni ile iliyotolewa chini ya Sheria ya Mbegu;

"muuzaji wa mbegu" maana yake ni wazalishaji, waingizaji nchini, wasafirishaji nje ya nchi, wachakataji, wauzaji, wasambazaji wa mbegu, wamiliki wa maabara za upimaji mbegu au mtu yeyote anayeshughulika na mbegu; na

"mwanasayansi" maana yake ni mtu ambaye anafanya utafiti wa kisayansi au kitaaluma kwa lengo la kugundua au kuthibitisha ukweli kwa manufaa ya jamii.

## SEHEMU YA PILI
## USAJILI WA WATOA HUDUMA ZA UTAFITI WA KILIMO NA MIRADI YA UTAFITI

### *(a) Usajili wa Watoa Huduma za Utafiti wa Kilimo*

Usajili wa watoa huduma za utafiti wa kilimo

**4**.-(1) Maombi ya usajili kama mtoa huduma wa utafiti wa kilimo yatawasilishwa kwa Taasisi kwa kujaza Fomu Na. 1A kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi yaliyotajwa chini ya kanuni ndogo (1) yanapaswa kuambatishwa na-

(a) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi isiyorejeshwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(b) wasifu;
(c) picha ya hivi karibuni ya pasipoti kwa njia ya kielektroniki;
(d) barua ya utambulisho, kama itahitajika;
(e) taarifa au nyaraka nyingine yoyote kama ambavyo Taasisi inaweza kuhitaji;
(f) cheti cha kitaaluma kilichothibitishwa; na
(g) cheti cha usajili wa kampuni, kama kitahitajika.

(3) Mwombaji wa usajili anapaswa kulipa kwa Taasisi ada ya usajili kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Uamuzi wa maombi

**5**.-(1) Taasisi, ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokea maombi chini ya kanuni ya 4, itafanya uamuzi wa maombi, na ambapo-

(a) maombi yamekubalika, itamjulisha mwombaji kwa maandishi kulipa ada ya usajili; au
(b) maombi yamekataliwa, Taasisi, ndani ya siku ishirini na moja tangu tarehe ya uamuzi, itamjulisha mwombaji kwa maandishi sababu za kukataliwa.

(2) Baada ya kulipa ada ya usajili, mwombaji atasajiliwa, atapewa cheti cha usajili na cheti cha uendeshaji kwa njia iliyoainishwa katika Fomu Na. 1B na 1C Jedwali la Kwanza.

(3) Cheti cha uendeshaji kilichotolewa chini ya kanuni ndogo ya (2), kitakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitatu na kinaweza kuhuishwa.

(4) Mwenye cheti cha uendeshaji atapaswa kuonyesha cheti hicho mahali kinapoonekana wazi katika eneo la kazi, na cheti hicho hakitaweza kuhamishwa umiliki wake.

(5) Ikiwa maombi yamekataliwa kutokana na makosa au mapungufu yanayoweza kurekebishwa, mwombaji anaweza kuwasilisha upya maombi hayo kwa masharti yatakayoelekezwa na Taasisi.

Ada ya kuhuisha cheti cha uendeshaji

**6**. Mtoa huduma wa utafiti wa kilimo aliyesajiliwa, baada ya miaka mitatu na mara baada ya kulipa ada iliyoainishwa katika Jedwali la Pili, anaweza kuhuisha cheti cha uendeshaji.

Rejesta ya watoa huduma za utafiti wa kilimo

**7**.-(1) Taasisi itatunza rejesta ya watoa huduma za utafiti wa kilimo kwa namna iliyoainishwa katika Fomu Na. 1D katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa madhumuni ya kuhuhisha rejesta, mtoa

huduma ya utafiti wa kilimo aliyesajiliwa atatoa taarifa kwa Taasisi kuhusu mabadiliko yoyote ya taarifa zake zilizowekwa kwenye rejesta.

*(b) Usajili wa Miradi ya Utafiti wa Kilimo*

Utaratibu wa usajili na uidhinishaji miradi ya utafiti wa kilimo na watafiti katika sekta binafsi

**8**.-(1) Isipokuwa miradi ya utafiti ambayo imeandaliwa na kutekelezwa kwa pamoja na muombaji na Taasisi, muombaji anayetaka kutekeleza mradi wa utafiti lazima awasilishe maombi yake kwa Taasisi kwa njia iliyoainishwa katika Fomu Na. 1E katika Jedwali la Kwanza.

(2) Mtafiti kutoka nje ya nchi, pamoja na mahitaji yaliyoainishwa kwenye kanuni ndogo ya (1), atawasilisha -

(a) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi isiyorejeshwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili;
(b) andiko lote la mradi;
(c) uthibitisho wa ufadhili wa mradi;
(d) uthibitisho wa mtafiti mwenyeji aliyesajiliwa;
(e) wasifu wa mtafiti kiongozi; na
(f) nyaraka au taarifa nyinginezo yoyote ambayo Taasisi inaweza kuhitaji.

Uchambuzi wa andiko

**9**.-(1) Andiko la mradi la utafiti litachambuliwa ili kubaini kama mradi unatimiza malengo yanayotarajiwa, njia, matokeo, maadili na viwango vingine vya tafiti za kisayansi.

(2) Uchambuzi wa andiko utafanywa na Kamati ya Kitaifa ya Maadili ya Utafiti wa Kilimo na baada ya kujiridhisha kuwa andiko lina sifa zinazohitajika, litasajiliwa.

(3) Ikiwa andiko limekataliwa, waombaji watapewa taarifa kwa maandishi pamoja na sababu zake.

(4) Taasisi, baada ya usajili wa mradi wa utafiti, itatoa cheti cha maadili kwa muombaji kulingana na Fomu Na. 1F iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza, na nakala ya cheti itawasilishwa kwa mamlaka husika inayowajibika kuratibu utafiti huo nchini ili kupata kibali cha utafiti.

(5) Isipokuwa kwa miradi ya utafiti ambayo imeandaliwa na kutekelezwa kwa pamoja baina ya muombaji na Taasisi, mtafiti ambaye mradi wake wa utafiti umepewa kibali cha utafiti chini ya kanuni ndogo (4) lazima alipe ada ya usajili wa mradi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(6) Baada ya kulipa ada ya usajili wa mradi chini ya kanuni ndogo ya (5), Taasisi itatoa barua ya utambulisho kwa mamlaka husika ambapo mradi utatekelezwa.

(7) Mtafiti ambaye anataka kufanya marekebisho katika mradi wa utafiti wa awali lazima, baada ya kuwasilisha sababu za kutosha kwa maandishi, aombe idhini ya Taasisi kufanya marekebisho.

Kuongeza muda

**10**.-(1) Mtafiti anayetaka kuongeza wigo au kushindwa kukamilisha mradi wa utafiti ndani ya muda uliowekwa katika andiko la utafiti, atawasilisha maombi kwa Taasisi kwa ajili ya kuongeza wigo au muda na atapaswa kuainisha sababu za kutosha kama ilivyoainishwa katika Fomu Na. 1G ya Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya kuongeza muda wa kutekeleza mradi wa utafiti lazima yawe yameambatishwa na uthibitisho wa malipo ya ada ya kuongeza wigo au muda kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Baada ya kulipa ada iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2), maombi ya kuongeza wigo au muda yatakubaliwa au kukataliwa na taarifa itatolewa kwa muombaji kama ilivyoainishwa katika Fomu Na. 1H ya Jedwali la Kwanza.

(4) Endapo maombi yaliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (2), yamekataliwa muombaji atajulishwa sababu za maombi hayo kukataliwa.

Rejesta ya miradi ya utafiti wa kilimo

**11**.-(1) Taasisi itatunza rejesta ya miradi ya utafiti wa kilimo kwa namna iliyoainishwa katika Fomu Na. 1D ya Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa lengo la kuhuisha rejesta, mtafiti atatakiwa kuijulisha Taasisi kuhusu mabadiliko yoyote ya taarifa zilizoingizwa katika rejesta.

Mradi wa utafiti wa taasisi ya umma

**12**.-(1) Chuo Kikuu au taasisi ya utafiti haitalazimika kuwasilisha maombi ya usajili ili kutekeleza mradi wa utafiti wa kilimo.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), chuo kikuu au taasisi ya utafiti itawasilisha kwa Taasisi orodha ya miradi ya utafiti wa kilimo iliyofanyika na muhtasari wa matokeo yake kila baada ya miezi sita au kama itakavyoamuliwa na Taasisi mara kwa mara.

Kuwasilisha ripoti za utafiti

**13**.-(1) Mwenye kibali cha utafiti atapaswa kuwasilisha kwa Taasisi -

(a) ripoti ya maendeleo ya kila mwaka;

(b) ripoti ya mwisho ya mradi ndani ya miezi sita toka

tarehe ya kukamilika kwa mradi wa utafiti; na

(c) ripoti au matokeo mengine kwa namna na wakati kama ambavyo Taasisi itaelekeza.

(2) Mwenye kibali cha utafiti ambaye anakiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) anatenda kosa.

## SEHEMU YA TATU
## TAARIFA NA TAKWIMU ZA UTAFITI WA KILIMO

Utunzaji na usalama wa takwimu

**14**.-(1) Taasisi itatunza takwimu na taarifa zote zinazohusiana na utafiti wa kilimo na inaweza, kutoa takwimu na taarifa hizo kwa mtu mwingine kwa maombi.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kutoa takwimu ya utafiti wa kilimo ambayo imeainishwa kama takwimu siri bila kuomba ruhusa kwa Taasisi.

(3) Mtu anayekiuka au anaeshidwa kuzingatia kanuni hii anatenda kosa na atakapopatikana na hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano lakini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita.

Kuanzisha mfumo wa taarifa jumuishi

**15**.-(1) Taasisi itaanzisha mfumo wa takwimu jumuishi kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za miradi ya utafiti.

(2) Mtafiti atawasilisha taarifa kwenye mfumo wa takwimu jumuishi wa Taasisi.

(3) Taasisi itahifadhi taarifa za miradi ya utafiti kwenye mfumo wa takwimu jumuishi bila kubadilisha majina ya vipengele vya takwimu zilizopo.

(4) Taasisi itakuwa na jukumu la kuhakikisha usalama wa takwimu na taarifa zilizohifadhiwa, kwa kutumia njia za usalama wa takwimu.

(5) Taasisi itatoza ada ya kupata taarifa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(6) Mtu atakayekiuka au asiyezingatia kanuni hii anatenda kosa.

## SEHEMU YA NNE
## MFUKO WA MAENDELEO YA UTAFITI WA KILIMO

Matumizi ya Mfuko wa Maendeleo ya Utafiti wa Kilimo
Sura ya 51

**16**. Kwa kuzingatia kifungu cha 26(2) cha Sheria, fedha zilizohifadhiwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Utafiti wa Kilimo zitatumika kwa kufadhili-

(a) utafiti wa kimkakati;

(b) uzalishaji na usambazaji wa mbegu kwa mazao ya

kimkakati;

(c) kuendeleza ujuzi na sayansi mpya katika sekta ya kilimo;

(d) miundombinu na vitendea kazi vya utafiti;

(e) uendelezaji wa biashara ya bidhaa zinazotokana na utafiti ili kuwezesha utoaji wa huduma za kimkakati; na

(f) huduma nyinginezo zinazohusiana na utafiti na maendeleo katika kilimo.

Kuanzishwa kwa Kamati

**17**.-(1) Mfuko wa Maendeleo ya Utafiti wa Kilimo utasimamiwa na Kamati ambayo itajumuisha-

(a) mkurugenzi anayehusika na utafiti kutoka ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na Fedha;

(c) mkurugenzi anayehusika na maendeleo ya mazao kutoka Wizara inayohusika na Kilimo;

(d) mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(e) mjumbe anayewakilisha Taasisi za Elimu ya Juu zinazohusika na kilimo.

(2) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Katibu wa Kamati.

(3) Kamati itasimamia taratibu za mikutano yake.

(4) Taasisi itahudumu kama Sekretarieti ya Kamati.

(5) Wajumbe wa Kamati chini ya kanuni ndogo ya (1) watahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu ambacho kinaweza kuongezwa kwa muhula mmoja zaidi.

Majukumu ya Kamati

**18**. Majukumu ya Kamati yatakuwa-

(a) kupokea, kujadili, na kutoa mapendekezo kwa Bodi kuhusu bajeti ya kila mwaka;

(b) kupitia taarifa za utekelezaji;

(c) kuhakikisha kuwa fedha zilizohifadhiwa katika Mfuko zinatumika kufikia malengo ya Mfuko;

(d) kuhakikisha kuwa shughuli za Mfuko zinafanyika ili kuleta tija na ufanisi;

(e) kusimamia upatikanaji wa fedha na kupendekeza vyanzo vipya vya fedha; na

(f) majukumu mengine yanayohusiana ambayo Kamati itaona ni muhimu.

Akaunti na Ukaguzi wa

**19**.-(1) Taasisi itahakikisha inatunza na kuhifadhi akaunti maalum ya benki na vitabu vya mahesabu kuhusiana

Mfuko

na:

(a) fedha zote zilizopokelewa na kutumika na Mfuko;
(b) taarifa ya mapato na matumizi ya Mfuko;
(c) vitabu vya mahesabu vya Mfuko vitakuwa sehemu ya mfumo wa mahesabu wa Taasisi na kukaguliwa mwishoni mwa kila mwaka wa fedha na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

(2) Taasisi itatenga kiasi cha fedha kisichozidi asilimia tano ya mapato ya kila mwaka kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

Kuwasilisha malalamiko

**20**.-(1) Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na kosa la kitaalam la mtoa huduma za utafiti wa kilimo aliyesajiliwa ikiwa moja kwa moja au vinginevyo anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Taasisi.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Taasisi inaweza, kwa utashi wake kuanzisha uchunguzi dhidi ya mtu ambaye tabia yake inalalamikiwa au baada ya kupokea taarifa kuhusu tuhuma za kosa la kitaalamu kuhusiana na mtoa wa huduma za utafiti wa kilimo aliyesajiliwa.

(3) Baada ya kupokea malalamiko, Taasisi itafanya yafuatayo-

(a) kuandika malalamiko dhidi ya jina la mlalamikiwa husika kama lilivyo katika rejesta; na
(b) kusoma na kuchambua malalamiko yaliyopokelewa ili kubaini kama kuna ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma.

(4) Taasisi baada ya kuzingatia malalamiko yaliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (3) inaweza-

(a) kuunda kamati ya uchunguzi, ikiwa inaamini kuwa kuna ukiukwaji wa maadili ya kitaalam; au
(b) kukataa malalamiko, ikiwa inaamini kuwa malalamiko hayo hayajumuishi ukiukwaji wa maadili ya kitaalam.

(5) Kamati ya Uchunguzi itaundwa na wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano.

(6) Kamati ya Uchunguzi inaweza, baada ya mashauriano na Taasisi, kuongeza mtu yeyote mwenye sifa za lazima ambazo zinaweza kusaidia katika kufanya uamuzi wa haki katika uchunguzi.

(7) Kamati ya Uchunguzi itatakiwa kukamilisha

*TANGAZO LA SERIKALI NA 448S (Linaendelea)*

mchakato wa uchunguzi ndani ya kipindi cha siku sitini tangu tarehe ya kuanza kwake isipokuwa kama imezuiliwa kwa sababu za kuridhisha.

Kukataa malalamiko

**21**. Taasisi inaweza kukataa malalamiko ambayo-

(a) yametolewa kwa njia ya mdomo; au

(b) yametolewa kwa maandishi lakini hayana ushahidi; au

(c) madai yake ni sawa na malalamiko ambayo yalishawahi kulalamikiwa na mlalamikaji huyo na kutolewa uamuzi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Ukomo wa muda

**22**.-(1) Isipokuwa ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2), malalamiko lazima yawasilishwe ndani ya miezi kumi na mbili baada ya-

(a) tarehe ambayo madai yanayohusisha suala linalolalamikiwa lilifanyika; au

(b) tarehe ambayo madai ambayo ni suala linalolalamikiwa lilifahamika kwa mlalamikaji.

(2) Ukomo wa muda katika kanuni ndogo ya (1) hautatumika pale ambapo Taasisi, baada ya maombi yaliyoandikwa na mlalamikaji, imejiridhisha kuwa mlalamikaji alikuwa na sababu za msingi za kutokuwasilisha malalamiko kwa wakati.

Mahudhurio ya pande husika

**23**.-(1) Kamati ya Uchunguzi itawajulisha wahusika kwa maandishi siku, tarehe, saa na mahali ambapo uchunguzi utafanyika kabla ya kuanza kusikilizwa.

(2) Mahudhurio mbele ya Kamati ya Uchunguzi yanaweza kufanywa na Mhusika mwenyewe, mwakilishi wake, wakala anayetambulika au wakili aliyeteuliwa kwa niaba yake kufanya hivyo, isipokuwa, kwa sababu za msingi Taasisi inaweza kuhitaji mhusika kuhudhuria mwenyewe.

(3) Kamati ya Uchunguzi inaweza, kuamuru uchunguzi ufanyike faraghani ikiwa hali ya suala linalolalamikiwa inaruhusu kufanya hivyo.

Uwasilishaji wa hati ya mashtaka

**24**.-(1) Kamati ya Uchunguzi kwa kuzingatia kanuni ya 20(4)(a) itaandaa hati ya mashtaka na kutoa notisi kwa mtoa huduma za utafiti wa kilimo kuhusu tarehe, saa na mahali ambapo uchunguzi utafanyika.

(2) Notisi na hati ya mashtaka zitatumwa kwa mtoa huduma za utafiti wa kilimo au mwakilishi wake kwa njia mkono, sanduku la posta lililosajiliwa, au mawasiliano ya

kielektroniki kwa anuani yake ndani ya siku kumi na nne kabla ya tarehe ya uchunguzi.

(3) Notisi na hati ya mashtaka itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

Usikilizaji wa malalamiko

**25**.-(1) Kamati ya Uchunguzi wakati inaanza kusikiliza shauri itamsomea mtoa huduma za utafiti wa kilimo hati ya mashtaka na kurekodi majibu yake.

(2) Endapo mtoa wa huduma za utafiti wa kilimo aliyesajiliwa ametoa jibu la kutokuwa na hatia, Kamati ya Uchunguzi itamtaka mlalamikaji kuwasilisha ushahidi kuthibitisha madai au pale ambapo Kamati ya Uchunguzi itakapobaini vinginevyo, itasoma ushahidi uliowasilishwa na mlalamikaji na kuhitaji utetezi kutolewa kuhusu suala hilo.

(3) Endapo mtoa huduma za utafiti wa kilimo aliyesajiliwa ameshindwa kuhudhuria kwenye uchunguzi au kujitetea bila sababu ya msingi na Kamati ya Uchunguzi imejiridhisha kuwa notisi imemfikia kikamilifu, Kamati ya Uchunguzi inaweza kuendelea na uchunguzi bila uwepo wake.

(4) Kamati ya Uchunguzi inaweza kuita shahidi yeyote na kumhitaji mtu yeyote kuwasilisha nyaraka yoyote aliyonayo kwa ajili ya uchunguzi.

Matokeo na mapendekezo

**26**.-(1) Kamati ya Uchunguzi itapaswa, ndani ya siku thelathini tangu kupokea malalamiko, kuchambua malalamiko hayo na kurekodi matokeo na mapendekezo.

(2) Kamati ya Uchunguzi itawasilisha matokeo na mapendekezo kwa Taasisi ndani ya siku kumi na nne baada ya kumaliza uchunguzi.

Uamuzi wa Taasisi

**27**.-(1) Taasisi inaweza, baada ya kupokea matokeo na mapendekezo ya Kamati ya Uchunguzi na ikiwa mashtaka yamethibitishwa kuwa ya kweli-

(a) kufuta usajili wa mtoa huduma za utafiti wa kilimo;

(b) kutoa amri ya kumsimamisha mtoa huduma za utafiti wa kilimo aliyesajiliwa kwa muda unaofaa kama ambavyo Taasisi inaweza kuona inafaa, ilimradi muda wa kusimamishwa usizidi miaka miwili; au

(c) kumuonya, kumkemea, kumrekebisha au vinginevyo mtoa huduma za kilimo aliyesajiliwa.

(2) Mkurugenzi Mkuu atapaswa, ndani ya siku saba baada ya uamuzi wa Taasisi, kuwataarifu pande husika kuhusu

uamuzi na sababu za uamuzi huo.

(3) Uamuzi uliofanywa na Taasisi utaanza kutekelezwa tangu tarehe uliyotolewa.

(4) Mmiliki wa cheti cha usajili kama mtoa huduma za utafiti wa kilimo ambaye usajili wake umefutwa kulingana na kanuni hii atapaswa, ndani ya siku saba, kurejesha cheti kwa Taasisi.

(5) Bila kujali ujumla wa masharti yaliyotangulia, Taasisi inaweza kumsimamisha mtoa huduma za utafiti wa kilimo aliyesajiliwa wakati malalamiko yake yanaendelea kushughulikiwa.

Kumbukumbu za mwenendo wa mashauri

**28**. Mwenendo wa mashauri ya Kamati ya Uchunguzi utarekodiwa kwa maandishi au aina nyingine yoyote ya kurekodi, na unaweza kuandikwa na mtu aliyeteuliwa na Taasisi kwa kusudi hilo na utahifadhiwa kama kumbukumbu sahihi ya Uchunguzi, endapo kikao kilifanyika faraghani, wajumbe waliohudhuria watakubaliana njia ya kurekodi mwenendo wa mashauri.

Rufaa kwa Waziri
Sura ya 51

**29**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, mtu ambaye ajaridhika na uamuzi wa Taasisi anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku ishirini na moja tangu tarehe ya kupokea nakala ya uamuzi.

(2) Rufaa kwa Waziri itawasilishwa kwa maandishi na itakuwa na-

(a) tarehe, jina, anwani, na sahihi ya mlalamikaji;
(b) maelezo ya malalamiko husika, sababu za rufaa na nafuu zinazotafutwa; na
(c) maelezo ziada au nyaraka nyingine yoyote ambayo mamlaka ya rufaa inaweza kuainisha.

Uwasilishaji wa rufaa

**30**. Mrufani anapaswa, ndani ya siku saba baada ya kukata rufaa, kutuma nakala kwa mjibu rufaa na wahusika wengine katika shauri la msingi, ikiwa wapo.

Uthibitisho wa uwasilishaji wa nyaraka

**31**. Endapo nyaraka yoyote inahitajika kutumwa kwa mtu yeyote, nyaraka hiyo inaweza kutumwa kwa mkono au sanduku la posta lililosajiliwa.

Mamlaka ya Waziri

**32**. Waziri anaweza, katika kushughulikia rufaa-

(a) kuthibitisha, kubatilisha, au kubadilisha uamuzi wa Taasisi;
(b) kurudisha shauri kwa Taasisi na maelekezo

yanayofaa;
(c) kuagiza Taasisi kufanya shauri upya; na
(d) kutoa amri yoyote inayohitajika kulingana na hali itakavyokuwa.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MBALIMBALI

Uzalishaji na matumizi ya mbegu

**33**. Kwa madhumuni ya kuongeza tija katika kilimo, Taasisi inaweza-
(a) kuzalisha, kusambaza na kuuza madaraja yote ya mbegu zinazozalishwa na Taasisi; au
(b) kuingia makubaliano na wafanyabiashara wa mbegu na kuwapa haki ya kupata na kutumia aina za mbegu zilizolindwa kisheria kwa kulipa mirahaba.

Jukwaa la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo
Sura ya 51

**34**.-(1) Jukwaa la Taifa la Ushauri wa Utafiti wa Kilimo kama lilivyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria litafanya shughuli zake kulingana na taratibu zilizoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi.
(2) Taasisi itagharamia shughuli za Jukwaa.

Makosa na adhabu

**35**. Mtu atakayetenda kosa chini ya Kanuni hizi na akipatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1A

---

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1) na (2))*

**FOMU**

**MAOMBI YA KUJISAJILI KAMA MTOA HUDUMA YA UTAFITI WA KILIMO**

1. Jina kamili la Mtu au Taasisi ………………………………………………...
2. Uraia……………………………….
3. Nchi atokayo...............................
4. Kijiji/Mtaa……………Kata…………
   Mji/Jiji…………Wilaya……………Mkoa……………………

| Weka picha hapa |
|---|

5. Anuani.................................................................................
6. Namba ya simu...........................
7. Barua pepe………………………….
8. Taasisi atokayo (umma/binafsi) ……………..………………………………...
9. Majina ya wadhamini na anuani (wadhamini wawili, mmoja lazima awe na anaishi Tanzania-

   (i) Jina kamili…………………………

   Simu……………………………….
   Barua pepe…………………………
   Mahali anapoishi………………….
   Uhusiano…………………………..

   (ii) Jina kamili…………………………

   Simu……………………………….
   Barua pepe…………………………
   Mahali anapoishi………………….
   Uhusiano…………………………
10. Uanachama katika chama cha kitaaluma (kama kipo):

   (i) ……………………………………………………………

   (ii) ……………………………………………………………

**UTHIBITISHO**

Mimi/sisi ……………………………………… nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli kwa mujibu wa uelewa wangu/wetu.

Jina…………………………………………

Wadhifa…………………………………..

Saini……………………………………………….

Imekwa sahihi leo tarehe ……….mwezi…………mwaka 20……..

**Ambatisha vitu vifatavyo***: Stakabadhi ya ada ya maombi, Wasifu; Barua ya utambulisho, kama inahitajika, Cheti cha usajili wa kampuni, kama kinahitajika, vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa, Nakala ya kitambulisho cha Taifa (Kwa raia wa Tanzania tu) au Hati ya Kusafiria.*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1B

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2))*

**CHETI CHA USAJILI KAMA MTOA HUDUMA YA UTAFITI WA KILIMO**

Hii ni kuthibitisha kwamba ………………….........................................amepewa cheti cha usajili kama mtoa huduma ya utafiti wa kilimo ndani ya Tanzania Bara kuanzia ………………………hadi…………………….

Imesainiwa na kuwekwa lakiri kwa niaba ya Taasisi na-

Jina.................................................................

Wadhifa........................................................

Sahihi............................................................

LAKIRI

Imewekwa sahihi leo terehe…………..mwezi …………,mwaka 20……

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1C

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2))*

**CHETI CHA UENDESHAJI CHA KUTOA HUDUMA ZA UTAFITI WA KILIMO**

Hii ni kuthibitisha kwamba, ………………….......................................amepatiwa cheti cha uendeshaji (kipya/kilichohuishwa) kama mtoa huduma ya utafiti wa kilimo ndani ya Tanzania Bara kuanzia tarehe….. mwezi ..................... mwaka 20…... na kufikia ukomo wake tarehe …… mwezi ..................... mwaka 20…..

Imesainiwa na kuwekewa lakiri kwa niaba ya Taasisi na-

Mkurugenzi Mkuu
Saini...........................................................

Imewekwa sahihi leo Tarehe……mwezi………mwaka 20……

LAKIRI

*TANGAZO LA SERIKALI NA 448S (Linaendelea)*

FOMU NA. 1D

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1))*

**REJESTA YA WATOA HUDUMA YA UTAFITI WA KILIMO**

| Na. | JINA | URAIA | NAMBA YA KITAMBULISHO CHAURAIA(NIDA) | NAMBA YA USAJILI | TAREHE YA USAJILI | ENEO LA UBOBEZI | TAASISI/BINAFSI | ANUANI | NAMBA YA SIMU | BARUA PEPE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1E

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 8(1))*

**MAOMBI YA USAJILI WA MIRADI YA UTAFITI WA KILIMO**

**1. Taarifa za Mtafiti/Watafiti**

*Ijulikane kwamba miradi inayojumuisha wageni kutoka nje ya nchi, inapaswa kuwa na angalau mtafiti mwenza mmoja ambaye ni mtanzania.*

**Taarifa za Mtafiti Kiongozi**

(a) Jina ……………………………………………………...………………
(b) Taasisi anayotokea………………………..……………………….
(c) Anuani ya Posta ………………………………………….....………
(d) Anuani ya Makazi ………………………………………….....…….
(e) Barua Pepe……………………………………………....................
(f) Simu/Simu ya Kiganjani……………………………........................
(g) Namba ya Utambulisho……………………………………………
(h) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) (Kwa Raia ………..…

**Taarifa za Mtafiti Mwenza**

(a) Jina la Mtafiti Mwenza ……………………………............................
(b) Taasisi anayotokea………………………...……………………….
(c) Sanduku la Posta…………………………………...………………
(d) Anuani ya Makazi ……………………………….....…………….
(e) Barua Pepe…………………………………..................................
(f) Simu/Simu ya Kiganjani……………………………........................
(g) Namba ya Utambulisho…………………………..………………..
(h) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) (Kwa Raia) …………

**Malizia na ambatisha taarifa za watafiti wenza wote*

**2. Taarifa za Mradi**

(a) Jina la Mradi ……………………………...........................................

(Ambatisha nakala tatu za andiko la mradi ikiwa ni pamoja na muhtasari au muhtasari mahususi wa mradi)

*TANGAZO LA SERIKALI NA 448S (Linaendelea)*

(b) Mahali utafiti utakapofanyikia (taja maeneo yote katika Wilaya husika) …………………………

(c) Bajeti ya Mradi...........................................................................................

(d) Chanzo cha Fedha za Mradi………………………………...…………..

(e) Muda wa utekelezaji wa Mradi wa Utafiti…………………………..……

(f) Tarehe ya kuanza kwa Mradi wa Utafiti……………………………..…

(g) Tarehe ya kukamilika kwa mradi wa Utafiti……………………….…..

**UTHIBITISHO**

Mimi/Sisi ………………………………………………… nina/tunathibitisha kwamba, taarifa zote zilizotolewa hapo juu ni za kweli tupu kutokana na upeo wangu/wetu wa kufikiri.

Jina la Mtafiti Kiongozi…………………………..…………………

Saini ………………………Tarehe…………………….………….

Jina la Mtafiti Mwenza …………………………………………….
(Ni lazima ajaze sehemu hii kama Mtafiti Kiongozi ni raia wa kigeni).

Tarehe …………………… Sahihi……………………………………

**Ambatisha yafuatayo:**
*Stakabadhi ya ada ya maombi, andiko lote la mradi, ufadhili wa fedha za mradi, Ushahidi wa mtafiti wa ndani aliyesajiliwa, Wasifu wa Mtafiti Kiongozi; na nakala za vyeti vya usajili ambapo kwa mwombaji ambaye ni raia wa kigeni anapaswa kuambatisha nyongeza ya barua ya kujidhatiti na nakala za vyeti vya usajili wa Mtafiti Mwenza.*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1F

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 9(4))*

**CHETI CHA MAADILI KWA UTAFITI WA MIRADI YA KILIMO**

Hii ni kuthibitisha kwamba, .................................................... amekadhiwa cheti hiki kwa uzingatiaji wa maadili utekelezaji wa utafiti wa mradi wa kilimo leo tarehe…… mwezi..……… mwaka 20 …………
Kutekeleza mradi wa utafiti wa kilimo unaojulikana kama ………………………….…
Lengo kuu la mradi ni……………………………………………………………….……..
Eneo la utafiti …………………………………………………
Tarehe ya kuanza kwa mradi…………………………
Tarehe ya kumalizika kwa mradi………………...….

Imewekwa sahihi na lakiri kwa niaba ya Taasisi na:

LAKIRI

Mkurugenzi Mkuu...................................................

Saini................................................................

Imewekwa sahihi leo tarehe ……mwezi ……..................mwaka 20……

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1G

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 10(1)*

**MAOMBI YA NYONGEZA YA MUDA WA MRADI WA UTAFITI WA KILIMO**

1. Jina Kamili………............…………………………..……………...…..
2. Anuani ya Makazi……………………………………………………
3. Barua Pepe…..............................................................….......................
4. Namba ya Simu……………………………………………..…………..
5. Nyongeza ya muda wa utafiti kutoka tarehe …………..hadi tarehe..….
6. Jina la Mradi…………………………………………………………….
7. Lengo kuu la mradi…………………………………………...……
8. Namba ya usajili wa mradi………………………………………...…
9. Eneo/maeneo la/ya Utafiti ……………………………………………...
10. Sababu za nyongeza ya muda wa mradi……………………………..
11. Nyongeza ya bajeti, kama ipo (USD/TZS) …………………………….

Sahihi ya Mwombaji……………… Tarehe.……………………….

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1H

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 10(3))*

**NOTISI YA NYONGEZA YA MUDA WA MRADI WA UTAFITI WA KILIMO**

Hii ni kukutaarifu kwamba maombi yako ya nyongeza ya muda yamekubaliwa kwa muda wa ……… ………………..kuanzia tarehe…… hadi tarehe………au yamekataliwa na Taasisi kwa sababu………………kutekeleza mradi ujulikanao kama………………wenye namba ya usajili…………………………. .

Imewekwa sahihi na lakiri kwa niaba ya Taasisi na-

Jina.........................................................

Saini....................................................

Wadhifa................................................

LAKIRI

Imewekwa sahihi leo tarehe…..Mwezi …………Mwaka 20…..

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

FOMU NA. 1I

REJESTA YA MIRADI YA UTAFITI WA KILIMO

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 11(1))*

| N/A | JINA LA MRADI | NAMBA YA UTAMBULISHO WA MRADI | LENGO LA MRADI | JINA LA MTAFITI KIONGOZI | ENEO LA UTAFITI | TAREHE YA KUANZA KWA MRADI | TAREHE YA KUKAMILIKA KWA MRADI | MAWANDA YA UTAFITI | BAJETI (TZS/ USD) | MFADHILI WA KIFEDHA | HALI YA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2), (3), 6, 8(3), 9 (5), 10(2) na 15(5))*

## MUUNDO WA ADA

| **a.** | **Kipengele** | | **Awamu za Malipo** | **Ada ya Watafiti wa Ndani (TZS)** | **Ada ya Watafiti wa Nje (USD)** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya usajili wa mtoa huduma ya utafiti wa kilimo | | Mara moja | 20,000 | 100 |
| 2. | Usajili wa mtoa huduma ya utafiti wa kilimo | | Mara moja | 300,000 | 300 |
| 3. | Ada ya kuhuisha matumizi ya cheti cha mtoa huduma ya utafiti wa kilimo | | Kila baada ya miaka mitatu | 100,000 | 150 |
| 4. | Ada ya maombi ya usajili wa mradi wa utafiti | | Mara moja | 20,000 | 100 |
| 5. | Usajili wa mradi wa utafiti wa kilimo | | Kwa mradi | 2% ya bajeti ya mradi | 2% ya bajeti ya mradi |
| 6. | Ada ya nyongeza ya muda wa mradi wa utafiti | | Kwa mradi | 20,000 | 100 |
| 7. | Upatikanaji wa taarifa | | Mara moja | 500,000 | 1000 |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 24 (3))*

**NOTISI**

Prof/Dkt/Bw/Bi ………………………… wa……………………. (weka anuani).

Ninakutaarifu kwamba ninakusudia kuanzisha mchakato wa uchunguzi dhidi yako. Nakala ya hati ya mashtaka imeambatishwa.

Unatakiwa kuainisha kwa maandishi sababu za utetezi utakazotumia kwaajili ya utetezi na uwakilishi wako unapaswa kunifikia ndani ya siku kumi na nne tangu kupokea kwa Notisi hii.

Pia ninakutaarifu kuwa uwakilishi wako usiponifikia ndani ya muda ulioainishwa hapo juu nitaendelea na mchakato wa uchunguzi bila ya kutoa notisi ya ziada.

Tarehe: ………………

……..……………
Sahihi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi

Ninathibitisha kwamba nimepokea Notisi hii.

Tarehe: ………………………

…………………..…………
Sahihi ya Mtoa huduma ya Utafiti wa Kilimo

*TANGAZO LA SERIKALI NA 448S (Linaendelea)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILMO TANZANIA (TARI)

HATI YA MASHTAKA

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 24 (3))*

**KOSA:**

Kosa: …………………………………………………………………………….

**MAELEZO YA KOSA**

Prof/Dkt/Bw/Bi………………………………wa S.L.P…………………………… (Jina la Mji) kwa kuwa mtoa huduma ya utafiti wa kilimo, tarehe ya …………. Siku ya ………(mwezi)……………(mwaka) ulitenda……………………..……...

Tarehe: ………………………

…………….…………
Sahihi ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi

*TANGAZO LA SERIKALI NA 448S (Linaendelea)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA KILIMO

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI)

---

**JEDWALI LA NNE**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 34(1))*

TARATIBU ZA JUKWAA LA TAIFA LA USHAURI WA UTAFITI WA KILIMO

Uendeshaji wa jukwaa

**1**. Jukwaa litakuwa na mamlaka ya kusimamia taratibu zake na kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa Sheria.

Uchaguzi wa Mwenyekiti Msaidizi

**2**. Wajumbe wa Jukwaa katika mkutano wa kwanza watachagua mmoja ya wajumbe atakayekuwepo kuwa Mwenyekiti Msaidizi wa Jukwaa na ataendelea kuwa mjumbe atakayesimamia ofisi kwa kipindi cha miaka mitatu tangu siku ya kuchaguliwa, na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Mgongano wa kimaslahi

**3**.-(1) Mjumbe ambaye yupo katika mkutano wa Jukwaa au Kamati ya Jukwaa na wakati kuna jambo la kuzingatiwa, na jambo hilo linamhusu mjumbe huyo au mtu anayehusiana na mjumbe huyo au mtu aliekaribu au kwa nafasi yake binafsi ana maslahi ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja, kwa haraka iwezekanavyo baada ya kuanza kwa mkutano huo, ataweka wazi mgongano wake wa kimaslahi na hatopaswa isipokuwa kama Mwenyekiti wa Jukwaa ataelekeza vinginevyo, kuwa sehemu ya jambo lolote au mjadala kwa, kupiga kura, na suala lolote linalohusiana jambo hilo.

(2) Mgongano wa kimaslahi uliowekwa wazi katika aya ndogo (1), lazima urekodiwe kwenye muktasari wa kikao husika.

Muda wa wajumbe

**4**.-(1) Mjumbe atatumikia kwa kipindi cha miaka mitatu, isipokuwa kama uteuzi wake utatenguliwa na Mamlaka

ya uteuzi au atafikia ukomo kuwa mjumbe katika namna yoyote ile na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Sura ya 51

(2) Mjumbe yeyote aliyeteuliwa chini ya Sheria anaweza kujiudhuru katika nafasi yake kwa kutoa notisi ya maandishi kwa Mamlaka yake ya uteuzi na atakoma kuwa mjumbe kuanzia tarehe iliyoainishwa kwenye notisi, ikiwa hakuna tarehe iliyoainishwa kuanzia siku ambayo Mamlaka ya uteuzi imepokea notisi hiyo.

(3) Mjumbe aliyeteuliwa kwa nafasi ya ofisi yake, atakoma kuwa mjumbe endapo atahamishwa kutoka ofisi hiyo au hatokuwa tena kwenye nafasi itakayomwezesha kuteuliwa kuwa mjumbe wa Jukwaa.

Wajumbe mbadala

**5**. Endapo nafasi ya Mjumbe wa Jukwaa imeachwa wazi kabla ya muda wa mjumbe kuisha, Waziri atateua mtu mwingine kujaza nafasi iliyoachwa wazi, na atatumikia kwa kipindi kilichobaki.

Vikao vya Jukwaa

**6**.-(1) Mwenyekiti wa Jukwaa ataongoza vikao vyote vya Jukwaa.

(2) Endapo Mwenyekiti hayupo katika kikao cha Jukwaa, Mwenyekiti Msaidizi ataongoza kikao hicho.

(3) Endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawakuhudhuria kikao, mjumbe yeyote atachaguliwa na wajumbe kuwa Mwenyekiti wa kikao.

Akidi ya kikao

**7**.-(1) Akidi ya kikao cha Jukwaa itakuwa ni nusu ya wajumbe wote wa Jukwaa.

(2) Maamuzi yoyote ya jukwaa yatafikiwa kwa pamoja, isipokuwa kama kutakuwa na mitazamo tofauti uamuzi utaafikiwa kwa kupiga kura na endapo kura zitalingana Mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu.

Ripoti ya vikao vya Jukwaa

**8**.-(1) Katibu atapaswa kuandaa muhtasari wa kikao cha Jukwaa utakaosomwa na kuidhinishwa au kurekebishwa.

Sura ya 51

(2) Taarifa ya utekelezaji wa makubaliano au mapendekezo itawasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu kwa utekelezaji kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria.

(3) Mkurugenzi Mkuu atafanyia kazi makubaliano au mapendekezo ya Jukwaa na kuandaa taarifa itakayowasilishwa katika kikao kinachofuata cha Jukwaa.

*TANGAZO LA SERIKALI NA 448S (Linaendelea)*

Nafasi zilizowazi hazitaathiri mwenendo wa vikao

**9**. Uhalali wa vikao vyote vya Jukwaa hautaathiriwa na nafasi yeyote iliyowazi miongoni mwa wajumbe au kwa mapungufu yeyote katika uteuzi wao.

Notisi au maelezo

**10**. Notisi au nyaraka zilizotolewa na au kwa niaba ya Jukwaa zitatiwa saini na-

(a) Mwenyekiti, Katibu au afisa yeyote wa Jukwaa aliyeidhinishwa na Katibu kwa maandishi.

(b) Kikao cha Baraza, kitafanyika ndani ya siku kumi na nne, baada ya Katibu kutoa notisi endapo theluthi moja ya wajumbe wataomba kwa maandishi na kama kuna uharaka wa jambo lolote na haiwezekani kutoa notisi, kikao maalum kitaitishwa baada ya kutoa notisi fupi.

Dodoma, **HUSSEIN MOHAMED BASHE**
…………………., 2023 *Waziri wa Kilimo*